RISALA YA CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI NA AFYA TAWI LA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KWA MWENYEKITI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI – TAREHE 27 APRILI, 2026

Bwana Yesu Asifiwe,
Tumsifu Yesu Kristo,
Asallam Aleykum,
Nawasalimu Kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali – Weledi na Ubora,

Mhe, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu wa Baraza, Katibu Msaidizi wa Baraza, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo mbalimbali, Mawakili waandamizi wa mikoa mbalimbali, Wajumbe wa Baraza, Wageni Waalikwa, itifaki imezingatiwa.

Kwa heshima na taadhima ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kutupatia afya njema na kutuwezesha kuudhuria shughuli hii muhimu ya leo. Pia Halmashauri ya TUGHE Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatoa shukurani za dhati kwa **Mhe. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu wa Baraza na Katibu Msaidizi wa Baraza** kwa kuandaa Mkutano huu muhimu ambao upo kisheria pia kuruhusu kufanyika mkoani Arusha.

Mhe. Mwenyekiti, Chama cha Wafanyakazi TUGHE tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa uongozi uliopita wa TUGHE TAWI kwa kipindi chote cha miaka mitano walipokuwa wanatekeleza majukumu yao kiukweli juhudi zao tumeziona na zimeweza kuzaa matunda na kuboresha chama cha wafanyakazi wa TUGHE TAWI.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa tumepata uongozi mpya wa TUGHE TAWI la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunakuahidi tutaendeleza kuimarisha ushirikiano kati ya Watumishi, Wanachama na Menejimenti.

Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru na kukupongeza kwa jitihada zako mbalimbali ulizozifanya na unazoendelea kuzifanya kwa kuhakikisha unaboresha mazingira ya kazi ndani ya ofisi yetu ikiwemo; kuongezeka kwa Stahili za Watumishi, kupata chakula, Mafunzo Ndani na Nje ya Nchi kwa watumishi wa kada zote, Magari, Vitendea kazi Pamoja na Mavazi kwa sasa tunaonekana watanashati ofisi nzima.

Mhe. Mwenyekiti, tunaendelea kushukuru kwa ajili ya DUBWASHIKA LA KIMKAKATI katika upande wa matibabu watumishi wote wa OMMS pamoja na familia zetu tunapata matibabu ROYAL CLASS hatupangi foleni tena kama zamani tunashukuru sana mmetuheshimisha sana haswa kwenye familia zetu.

Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru kupeleka magari baadhi ya Ofisi za Mikoani ili ziwasaidie kuendelea kutoa huduma kwa wananchi na Serikali

kwa Ujumla lakini pia mwendelezo mzuri wa Ujenzi wa Majengo yetu ya Mikoani.

Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru kwa ajili ya Kliniki ya Sheria zinazoendelea kwenye Mikoa na Wilaya kwa ajili ya kutoa huduma ya Kisheria. Tumeona imeleta tija sana haswa kutangaza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile tunakushukuru Kliniki ya Sheria imekuwa ikishirikisha watumishi wote tulioko chini ya ofisi yako bila kujali kada na watumishi wengi wameshiriki katika kutoa huduma hiyo na haswa wakati wa Ufunguzi.

Mhe.Mwenyekiti, tunashukuru uwepo wa Ofisi za Mikoani za Mwanasheria Mkuu wa serikali lakini ni vema kuziongeza ili kuendelea kutoa huduma za kisheria kwa wananchi kwa urahisi zaidi. Ikikupendeza hata kila Mkoa kuwepo na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali na hapo baadae tufungue Ofisi za Wilaya. Kwa sasa wananchi wanatumia gharama kubwa sana kufuata huduma za kisheria hasa kwenye mikoa ambayo haina Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa shukrani nyingi na pongezi kwa viongozi na Menejiment nzima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa juhudi kubwa na zenye mafanikio za kuboresha hali ya kipato na kupandisha ari ya utendaji kazi kwa watumishi. Pia watumishi wanatoa shukrani kwa Menejimenti kutekeleza mpango wa mafunzo ambao umewezesha watumishi kupata mafunzo nje ya nchi kwa mwaka huu wa fedha baada ya muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, TUGHE tawi la ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikari, Bado tunaendelea kutembea na Kipaumbele chako nanukuu;

“Kipaumbele chako cha kwanza ni maboresho ya mishahara, kipaumbele cha pili ni maboresho ya mishahara na kipaumbele cha tatu ni maboresho ya mishahara mipya ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali”. Aidha watumishi wote wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wanaendelea kukuombea kwa Mwenyezi Mungu Vipaumbele vyako hivi viweze kutimia.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba kuwe na Bajeti ya kutosha kwenye sikukuu ya Mei Mosi ili pia iweze kuwapeleka baadhi ya Viongozi wa Halmashauri ya Tawi, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Mshindi wa Jumla wa Mfanyakazi Hodari kwenda kushiriki sherehe za Mei Mosi Pamoja na kwenda kupokea Zawadi yake Mbele ya Mgeni Rasmi ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kufanya hivi tutakuwa tumeweka morali na Motisha kwa watumishi wote kufanya kazi kwa bidii, utii, kujitoa na kufuata kanuni, taratibu za kazi mahala pa kazi.

Mhe.Mwenyekiti, Licha ya mafanikio makubwa katika mafunzo ya muda mfupi yaliyotolewa ndani na nje ya nchi kwa mwaka huu wa fedha, watumishi wanaomba mpango wa mafunzo ya muda mrefu uwianishwe na bajeti ya kila mwaka na kuwe na uwazi zaidi kwa kila Divisheni na Kitengo kuainisha

mapema orodha ya watumishi watakaonufaika na ufadhili wa mwajiri kushiriki mafunzo ya muda mrefu. Kwa sasa haiko wazi nani anaratibu au anamiliki utaratibu huu kwakuwa watumishi wamekuwa wakiambiwa hawapo kwenye mpango wa mafunzo na hawaaambiwi watakuwepo lini au utaratibu gani ufuatwe ili kuwepo kwenye mpango huo. Lakini pia kumekuwepo na sintofahamu juu ya nani hasa anahusika kwakuwa mara kadhaa watumishi wameelekezwa kumwona Afisa Bajeti wa Divisheni ambaye naye huwaelekeza Divisheni ya Utawala na Rasilimali Watu ambako pia hurejeshwa kwenye Divisheni au kitengo.

Mhe.Mwenyekiti, Watumishi wamelalamika kutokulipwa fedha za kujikimu wakiwa masomoni (stipend allowance) jambo ambalo linawaathiri na kuwapa mzigo mkubwa wa gharama. Watumishi wanaomba iwekwe wazi stahiki zao kwa mujibu wa kanuni za kudumu za utumishi ni zipi wanapokuwa masomoni na ziainishwe katika barua zao za ruhusa na kuzingatiwa na kutimizwa ipasavyo.

Mhe.Mwenyekiti, watumishi wanaomba dodoso la mafunzo liwekwe kwenye lugha mama ya Kiswahili kwa kuwa ni mpango wa miaka mitano ili kila mtumishi aijaze kwa ufasaha katika lugha mama, pia watumishi wanaomba kabla ya kujaza dodoso hilo yatolewe mafunzo ya siku moja ili kila mtumishi ajaze akiwa na uelewa wa nini anajaza, watumishi katika Divisheni ya Utawala wameomba hasa kada za udereva, masijala, wahudumu, walinzi na masekretali wazingatiwe kwenye mpango wa mafunzo kwa mwaka wa fedha ujao kwani karibu wote hawajapata mafunzo nje ya nchi ukiacha wawili wale wastaafu watarajiwa tu.

Mhe.Mwenyekiti, watumishi tunaomba mtumishi anapokuwa anastaafu Utumishi wa Umma haswa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunaomba mtumishi huyo apewe asante ya mwajiri kumshika mkono mstaafu.

Mhe.Mwenyekiti, Watumishi kutoka Divisheni ya DCAS hususani Mawakili walioanzia kazi Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) wanadai kutaarifiwa kuwa hawatapanda daraja sambamba na wenzao mwezi Julai 2026 kutokana na kukosekana kwa taarifa zao za utendaji kazi. Jambo hili limewashtua kwakuwa wakati wakiwa NPS wanadai walitaarifiwa na Divisheni pamoja na Idara ya Utawala na Rasilimali Watu kuwa hawana haja ya kujaza taarifa za kazi za NPS na kwamba kutokujaza huko kusingewaathiri. Mawakili wanaomba mwajiri aingilie kati suala hili ili kunusuru mawakili hawa kuachwa nyuma na wenzao katika upandaji madaraja mwaka huu.

Mhe.Mwenyekiti, Pamoja na Maombi hayo pia Halmashauri ya TUGHE Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tunapenda kukujulisha umuhimu wetu mahali pa kazi kwani tumekuwa msaada mkubwa kama kiunganishi kati ya Watumishi na Mwajiri, Pia tumekuwa tukitatua migogoro ya Wafanyakazi tukishirikiana na Mwajiri, Kutetea Maslahi ya Watumishi mahali pa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, TUGHE Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali tutaendelea kujivunia uwepo wako ndani ya Taasisi yetu kwani tunatarajia mambo makubwa yajayo ndani ya Ofisi yetu chini ya Uongozi wako, Mhe, Mwenyekiti chini ya uongozi wako umeboresha Imani na matumaini kwa Watumishi wote wa Ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, TUGHE Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu akupe afya njema na kukutunza kila utekelezapo majukumu yako katika kuitumikia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MUNGU IBARIKI OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI,
MUNGU IBARIKI TANZANIA

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI WELEDI NA UBORA